


# UQAB
Jarida la

*Toleo 17 - Ramadhan 1439 AH / June 2018 Miladi*


**Kuangazia Vita Vya Kwanza Na Pili**

**Kujikinga na Kutotosheka**

**Ndoa Chini ya Mfumo wa Kisekula wa Kirasilimali ni Taasisi ya Ulimbikizaji Mali**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 13**

**SWALI/JAWABU: Ziara ya Mohammad Bin Salman ya Uingereza, Amerika na Ufaransa**




## Tangazo la Matokeo ya Kuutafuta Mwandamo wa Mwezi wa Baraka wa Ramadhan wa Mwaka wa 1439 H


uqab.or.ke uqab_htk uqab_htk UQAB-Magazine-1911964012162253

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 23/1439 H | Ijumanne, 29 Sha'aban 1439 H | 15/05/2018 M

# Tangazo la Matokeo ya Kuutafuta Mwandamo wa Mwezi wa Baraka wa Ramadhan wa Mwaka wa 1439 H

**<u>Taarifa kwa Vyombo vya Habari</u>**

Najilinda na Allah kutokana na Shetani aliye laaniwa,

**شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِيَ أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ يُرِيدُ اللهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلاَ يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُواْ الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُواْ اللهَ عَلَى مَا هَدَاكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ**

"Mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uongofu na upambanuzi. Basi atakaye kuwa mjini katika mwezi huu naafunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu siku nyengine. Allah anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hisabu, na mumtukuze Allah kwa yale aliyowaongozeni kwayo ili mupate kushukuru." [Al-Baqara: 185]

Sifa njema zote zamstahiki Allah na rehma na amani zimshukie Mtume wa Allah, jamaa zake, maswahaba zake, washirika wake, na wale wanaofuata njia yake kwa kuifanya itikadi ya Kiislamu kuwa ndio msingi wa fikra zao na hukmu za kisheria kuwa kipimo cha vitendo vyao na chimbuko la maamuzi yao.

Al-Bukhari amepokea katika Sahih yake kutoka kwa Muhammad Bin Ziyad kwamba amesema: Nilimsikia Abu Hurairah (ra) akisema, "Mtume, rehma na Amani zimshukie yeye na jamaa zake, amesema, au alisema, Abu Al Qasim (saw) amesema:

**صوموا لِرُؤيتِهِ وأَفْطِرُوا لرؤيتِهِ فإنْ غُبِّيَ عليكم فأَكْمِلُوا عِدَّةَ شعبانَ ثلاثين**

"Fungeni kwa kuonekana mwezi na fungueni kwa kuonekana mwezi, na ikiwa kutakuwa na mawingu juu yenu (na kuwaziba kuuona mwezi), basi kamilisheni siku thalathini za Shaaban."

Baada kuutafuta mwandamo wa mwezi mpya wa Ramadhan iliyo barikiwa usiku huu, usiku wa kuamkia Jumatano, mwezi haujathibitishwa kuonekana kwa mujibu wa matakwa ya shari'ah, hivyo basi kesho, Jumatano, ni kukamilisha mwezi wa Shaaban InshaAllah, na Alhamisi, kesho kutwa, itakuwa ndio siku ya kwanza ya mwezi wa baraka wa Ramadhan…

Enyi Waislamu Wapendwa:

Mwezi huu wa baraka unawashukia juu yenu hali ya kuwa munashuhudia mataifa ya kikafiri yakiungana (na kutoa wito) kwa kila mmoja wao kutushambulia, pamoja na watawala waovu miongoni mwa watu wenyewe, wanaokimbilia kuwasaidia katika njama zao dhidi ya Uislamu na watu wake. Hili latukumbusha Hadith Sahih: Mtume (saw) amesema:

**يُوشِكُ الْأُمَمُ أَنْ تَدَاعَى عَلَيْكُمْ كَمَا تَدَاعَى الْأَكَلَةُ إِلَى قَصْعَتِهَا» فَقَالَ قَائِلٌ: وَمِنْ قِلَّةٍ نَحْنُ يَوْمَئِذٍ؟ قَالَ: «بَلْ أَنْتُمْ يَوْمَئِذٍ كَثِيرٌ وَلَكِنَّكُمْ غُثَاءٌ كَغُثَاءِ السَّيْلِ وَلَيَنْزَعَنَّ اللَّهُ مِنْ صُدُورِ عَدُوِّكُمْ الْمَهَابَةَ مِنْكُمْ وَلَيَقْذِفَنَّ اللَّهُ فِي قُلُوبِكُمْ الْوَهْنَ» فَقَالَ قَائِلٌ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، وَمَا الْوَهْنُ؟ قَالَ: «حُبُّ الدُّنْيَا وَكَرَاهِيَةُ الْمَوْتِ**

"Watu wataalikana kukushambulieni kama wanavyoalikana walaji kuishambulia sahani ya chakula. Mmoja akauliza: Je, hiyo itatokana na uchache wetu siku hiyo? Akajibu: La, bali siku hiyo mutakuwa wengi: lakini mutakuwa kama taka mithili ya taka zinazo sombwa na mvua, na Allah ataondoa hofu yenu katika vifua vya maadui zenu na atazigonga nyoyo zenu kwa al-Wahn. Mmoja akauliza: Ni nini al-Wahn? Mtume wa Allah (saw) akajibu: Kupenda dunia na kuchukia kifo."

Lakini tunajua kuwa Ramadhan ni mwezi wa subira; na subira ndio ufunguo wa afueni (kutokana na mateso). Tunakumbuka yale yaliyosimuliwa na al-Bukhari (rh): kutoka kwa Abu Abd Allah Khabbab ibn al-Arat (ra):

*Endelea Uk..3*



Email: info@uqab.or.ke

«شَكَوْنَا إِلَى رسولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم وَهُو مُتَوسِّدٌ بُردةً لَهُ في ظلِّ الْكَعْبةِ، فَقُلْنَا: أَلا تَسْتَنْصرُ لَنَا أَلا تَدْعُو لَنَا؟ فَقَالَ: قَد كَانَ مَنْ قَبْلَكُمْ يؤْخَذُ الرَّجُلُ فيُحْفَرُ لَهُ في الأَرْضِ فيُجْعَلُ فِيهَا، ثمَّ يُؤْتِى بالْمِنْشارِ فَيُوضَعُ علَى رَأْسِهِ فيُجعلُ نصْفَيْن، ويُمْشطُ بِأَمْشاطِ الْحديدِ مَا دُونَ لَحْمِهِ وَعظْمِهِ، مَا يَصُدُّهُ ذلكَ عَنْ دِينِهِ، واللَّهِ ليتِمنَّ اللَّهُ هَذَا الأَمْر حتَّى يسِير الرَّاكِبُ مِنْ صنْعاءَ إِلَى حَضْرمْوتَ لاَ يخافُ إِلاَّ اللهَ والذِّئْبَ عَلَى غنَمِهِ، ولَكِنَّكُمْ تَسْتَعْجِلُونَ»

“Tulimlalamikia Mtume wa Allah (saw) huku amejipumzisha katika kivuli cha nguo ya Ka’aba, na kumuuliza: kwa nini usituombee nusra kwa Allah? Kwa nini usituombee kwa Allah? Yeye (saw) akajibu: Hakika miongoni mwa wale waliokuwa kabla yenu alikuwa akichukuliwa mtu (muumini) akichimbiwa shimo akitiwa ndani yake. Kisha ukiletwa msumeno na kuekwa juu ya kichwa chake na kukatwa vipande viwili. Na kuchanwa kwa kichana cha chuma na nyama yake kunyofolewa kutoka katika mifupa yake, lakini, yote hayo hayakumfanya yeye kuachana na dini yake. Wallahi! Dini hii (Uislamu) itakamilika (na kupata ushindi) mpaka aliye juu ya kipando (msafiri) atatoka Sanaa (mji mkuu wa Yemen) kwenda Hadhramout haogopi chochote isipokuwa Allah na mbwa mwitu kwa mbuzi wake, lakini nyinyi muna pupa”.

Hii ni ahadi ya Allah ya izza na ushindi kwa Dini yake hata kama ni baada ya muda, na tunachotakiwa pekee ni tuwe na ikhlasi kwa Allah na kuwa na subira na ukakamavu katika kumtii Yeye (swt), na kuwa na dhana nzuri na matarajio ya kupata ahadi hiyo ya Allah pasi na shaka wala tashwishi. Na Allah havunji ahadi yake, Yeye ni Mkweli na ahadi yake ni ya kweli.

Sisi katika Hizb ut Tahrir tunaulingania Ummah wa Kiislamu kuchukua msimamo mkubwa, unaomridhisha Mola wake, na kuusafisha na kuukomboa kutokana na dhambi hili kubwa na khiyana kuu, msimamo utakaoondoa fedheha mabegani mwake, na kuregesha utukufu katika ardhi zake zote…

Tunawasihi Waislamu kuunganisha mikono yao (iliyo twahirishwa kwa udhu) pamoja na mikono yetu katika Hizb ut Tahrir, iliyomo ndani ya mvutano wa kifikra na mvutano mkali wa kisiasa. Inayofichua njama za kijanja za Wamagharibi, na kuwaonesha mstari ulionyoka wa Uislamu. Huenda Allah akapitisha kuwa kwa mikono yenu na yetu ushindi na izza zitakuja; kwa kusimama dola ya Khilafah Rashida katika njia ya Utume. Allah ajaaliye ushindi huu katika mikono ya Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa Ata Bin Khalil Abu Rashtah, na kwamba mumpe ahadi ya utiifu (Ba’yah) awe Khalifah na kutawala kwa Kitabu cha Allah na Sunnah za Mtume wake mwenye daraja (saw), na muishi ndani ya dola ya Khilafah inayotekeleza Shariah ya Allah, na mubebe ulinganizi wa Uislamu, mwenge wa uongofu kwa wanadamu wote…

Enyi maafisa wa majeshi ya Waislamu, jueni kuwa Allah ataipa ushindi Dini yake, ikiwa si kwa kupitia mikono yenu basi itakuwa kwa kupitia mikono ya wanaume wengine wenye ikhlasi ambao Yeye (swt) atawakirimu kwa izza, kwa hivyo musiikose hadhi hii kubwa na kusimama na Ummah ili kupata radhi za Allah kwa utukufu wa hapa duniani na kesho akhera.

Pia ni furaha yangu kuwafikishia salamu zangu na zile za Mkuu wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na wote wale wanaofanya kazi ndani yake kwa Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni maarufu Ata Bin Khalil Abu Rashtah, na kwa Waislamu wote kwa ajili ya mwezi huu wa baraka, nikimuomba Allah atuokoe na Moto wa Jahannam ndani ya mwezi wa rehma na toba, na tunamuomba Allah (swt) aturuhusu kuushuhudia Usiku wa Cheo (Laylatul Qadr) na kutubariki kwa malipo yake…

Ewe Allah, Mola wa Mbingu na Ardhi, tukirimu kwa kumpa Ba’yah Khalifah wa Waislamu katika Khilafah Rashida ya pili katika njia ya Utume, sasa au sasa hivi… Allahumma ameen ameen ameen.

Wassalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Kuamkia Jumatano ni tarehe 30Sha’ban mwaka wa 1439 H.

**Dkt. Osman Bakhach**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 10/1439 H | Ijumatano, 30 Sha'aban 1439 H | 16/05/2018 M

# Tunawapongeza Waislamu kwa Kuwasili kwa Mwezi wa Baraka wa Ramadhan

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Hizb ut Tahrir Kenya inafuraha sana kuwapongeza Waislamu nchini na ulimwengu wote kwa jumla kwa kuwasili kwa mwezi wa baraka wa Ramadhan. Tunapoingia katika mwezi huu wa rehma, toba na kuokolewa na Moto wa Jahannam, tunatoa wito kwa Waislamu matajiri nchini kusaidia kwa kuwapa sadaka ndugu zao na dada zao masikini hususan wale walioathirika na mafuriko.

Tunawakumbusha Waislamu wakati wanapofunga kuhakikisha wanafikia lengo lililotajwa na Allah (swt) ambalo ni uchaMungu, daraja ya juu kabisa kwa Muislamu inayomlazimisha yeye kushikamana na maamrisho ya Allah. Huku hivi leo tukiwa twaishi katika jamii huru ya kisekula ambayo yaitazama dini kama kadhia ya muda tu, twahitaji kupinga mtazamo huu fisidifu na hivyo basi Ramadhan inapasa kuwa mwezi wa Waislamu kuongeza kumkumbuka kwao Allah (swt) kuliko kuwa ni mwezi wa utiifu wa muda tu kwa maagizo Yake. Uislamu ni Dini iliyo kamilifu hivyo basi tunaamrishwa kutabikisha kwa ukamilifu maagizo ya Kiislamu yanayo husiana na mambo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Kwa hakika Ramadhan huleta kheri kwa Waislamu wote, lakini hali ya Umma hususan katika ulimwengu wa Kiislamu bado ingali mbaya na ya kutisha huku ukipitia njama ovu za maadui wa Uislamu. Hali nchini Syria inazidi kuzorota kutoka kuwa ni mbaya mpaka kuwa mbaya zaidi huku Amerika na washirika wake ikiwemo Urusi, Iran nk zikiishambulia kwa mabomu mchana na usiku! Waislamu wanaonja mateso haya mabaya katika nyanja zote za maisha kutokana na kukosekana utekelezwaji wa Qur'an katika maisha yao yote. Hivyo basi katika mwezi huu ulioteremka wahyi, tunawakumbusha kusoma Qur'an na kutafakari maana iliyo ndani yake na pia kushikamana imara na mafundisho yake. Wanaposoma Qur'an Tukufu, ndani ya mwezi huu uliofadhiliwa kwa yakini waelewe kuwa mateso haya yatamalizika tu pindi watakapo tabikisha moja ya majukumu ya lazima kupitia kusimamisha tena Khilafah kwa njia (manhaj) ya Utume katika mojawapo ya mataifa makuu ya Waislamu. Khilafah ndio dola pekee itakayo tabikisha sharia ya Quran katika nyanja zote za maisha na kwa hakika itang'oa utawala wa Amerika kwa kuyafurusha majeshi yake yanayoeneza ufisadi ardhini na hususan katika ardhi za Waislamu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Kuangazia Vita Vya Kwanza Na Pili

Ndani ya mwezi Mei, 1915 meli ya Uiengereza inayoitwa Lusitania ilipigwa mabomu na nyambizi (sub-marine) ya kivita ya Ujerumani. Kwa kuwa miongoni mwa abiria pia waliokuwamo wamarekani, Uingereza ilipatiliza kwa haraka na kwa uhodari mkubwa ilipatiliza fursa kuishawishi Marekani kujitosa katika Vita vya Kwanza vya Dunia. Aidha, ndani ya mwezi Mei 1945 ndio vilimalizika Vita Vya Pili Vya Dunia. Vita hivi viwili vya Kwanza na vya Pili ni matukio muhimu ya kitareekh ambayo Waislamu tunapaswa kujifunza kutokana nayo.

Vita ya kwanza vya dunia viliibuka ndani ya Ulaya kutokana na tabia ya mfumo wa kibepari wa kuzaa ugomvi wa kimaslahi, ushindani na shauku ya kila dola kujijengea himaya ya kimaslahi dhidi ya mwenziwe, na wakati mwengine kwa gharama ya dola nyingine.

Baada ya dola za Ulaya hususan Uingereza kuhisi Ujerumani imekuwa tishio na ina shauku kubwa ya kuchukua uongozi wa kiulimwengu na kuharibu maslahi yake na kuathiri himaya yake. Uingereza ikashirikiana na dola za Urusi na Ufaransa na pia kufanya kila linalowezekana kuishawishi Marekani, kwa ilikuwa ni dola yenye maendeleo makubwa ili ijitose ndani ya vita hivi dhidi ya Ujerumani. Hilo lilisukumwa pia na khofu ya Uingereza kutokana na nguvu kubwa ya Ujerumani kijeshi na kiteknolojia iliyotokamana na maendeleo makubwa iliyoyafikia kwa kuwekeza sana katika teknolojia na ufundi tangu mwaka 1870 yalipoanza Mapinduzi ya Viwanda.

Vita vya kwanza vilimalizika kwa kuandikwa zinazoitwa nukta 14 za mawafikiano ya amani baada ya vita (Versailles Treaty) na kwa dola zilizoshinda yakaunda Jumuiya ya League of Nations kwa lengo la kuusimamia na kuumiliki ulimwengu wakidai kuwa ni Jumuiya ya kudhamini amani ya ulimwengu.

Licha ya kuwepo kwa Jumuiya ya League of Nations iliyodaiwa kudhamini amani na usalama wa ulimwengu, Vita vya Pili vya Dunia viliibuka 1939 tena ndani ya Ulaya kama awali, hatimaye Marekani nayo ikashawishiwa na baada ya kuhisi kuna maslahi yake, chini ya Raisi Franklin Roosevelt ilijitosa vitani mwaka wa 1941.

Tofauti na Vita va Kwanza, katika vita hivi upepo ulikwenda dhidi ya mabwana wa dunia wa wakati ule ambao ni Uingereza na Ufaransa kwa kudhoofishwa sana kwa vita na pia kudhoofika haiba zao kimataifa kutokana na kampeni kali iliyoshamiri dhidi ya 'Ukoloni mkongwe' iliyopigiwa debe na Marekani na Urusi, na kwa kuwa madola yao ndiyo yaliyokuwa kwa kiasi kikubwa yakishikilia makoloni dunia nzima, ilikuwa rahisi kwa Marekani kuuleta uwanja wa kimataifa upande wake kwa mapana na marefu mara vilipomalizika vita katika mwaka 1945.

Vita hivi vinadhihirisha yafuatayo:

a. Hali ya siasa za kimataifa haikuganda, upo uwezekano wa kubadilika kutokana na hali ya ulimwengu.

b. Kunadhihirika ugomvi na husuma za kimaslahi baina ya madola ya kibepari

c. Kutofaa kwa Jumuiya za kibepari kama Umoja wa Mataifa kwa leo ambazo huvikwa guo la kudhamini amani na usala wa ulimwengi ilhali ni taasisi za kikoloni.

d. Kwa dola yenye mfumo kuupoteza uongozi wa kimataifa ni jambo la khatari, kwa kuwa huchukuwa muda kujipanga kuurejesha tena kama inavyohangaika Uingereza na Ufaransa leo katika hali ya kukata tamaa kutaka kurejesha nafasi zao.

e. Dola changa isiyo na mfumo ni khatari kwa kila hali, moja wapo hutumika kufinyanga na kupigania malengo ya dola kubwa, kama ilivyodhihirika katika vita hivyo hususan vya Pili namna zilivoshiriki nchi mbalimbali kwa niaba ya dola kubwa.

f. Dola katika kukabiliana na hali yoyote inabidi iwe makini, kwa kuwa inaweza kudhani tukio fulani litaweza kuinua haiba yake ilhali ikaporomoka. Mfano mzuri, dola ya Uingereza na Ufaransa hususan katika kukabiliana na Vita vya Pili.

**Masoud Msellem**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Tanzania**

# Kujikinga na Kutotosheka

وَأَمَّا مَن بَخِلَ وَاسْتَغْنَىٰ * وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَىٰ * فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْعُسْرَىٰ * وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى

"Na ama mwenye kufanya ubakhili na akajiona anajitosheleza, na akadhibisha lililo jema. Tutamsahilishia yawe mazito. Na mali yake yatamfaa nini wakati atakapokuwa anadidimia (katika maangamivu)? [Al-Lail: 8-11]

Ni kiwango gani cha mali kinachomtosheleza mwanadamu kuishi maisha ya furaha? Swali hili laweza kujibiwa kwa njia zaidi ya mia moja.

Ama Uislamu umemfanyia mwanadamu wepesi kwa kumuunganishia baina ya matarajio yake na matakwa ya Allah (swt). Allah (swt) amempa mwanadamu haki kamili kufanya jitihada za kujipatia kile anachoweza kukipata miongoni mwa vilivyo halalishwa, na katika historia yetu tuna mifano kadha wa kadha ya watu waliokuwa na utajiri mkubwa na kufurahia manufaa yake na kila fursa ya kutoa kwa ajili ya Allah ilipo wadia kamwe hawakufikiria mara mbili. Hili lawezekana tu ikiwa Muislamu atatambua kwamba saada (furaha) ya kikweli iko katika kupata radhi za Allah (swt) na jambo la pekee ambalo mwanadamu anastahili kutokinai nalo ni akhera.

Ukweli ni kuwa, kuporomoka kwa Waislamu kumetokana na kutotosheka na khiyana na nidhamu ya ulafi ya kirasilimali iliyo wageuza watu kuwa mashini za uchumaji pesa. Ni ulafi huu ndio uliomfanya Abdul Aziz ibn Saud kuuza Ummah wa Kiislamu na Akhera yake kwa makafiri. Na pia ni ulafi huu ndio unaowafanya watawala vibaraka kutekeleza uhalifu mbaya dhidi ya watu wao wasiokuwa na hatia. Huu ndio ulafi uliopelekea serikali ya Uturuki kuwatelekeza watu wa Syria kufa; ulafi uliolizuia jeshi la Pakistan kutoikomboa Kashmir; ulafi wa Wasaudi ndio uliotia fora zaidi. Ulafi wa utawala na pesa; huu ndio uliolemaza uongozi wa Waislamu.

Khalifah Umar Bin Abdul Aziz (rh) aliwahi kusema, "Moyo wangu kamwe haukinai mazuri yoyote ya ulimwengu unayopewa bali hutaka mazuri zaidi, na nilipopewa lile ambalo ni kubwa zaidi kuliko ulimwengu, moyo wangu ulilitamani hilo nalo ni, akhera." Ni vipi basi itakuwa miondoko ya watu wa kawaida ikiwa hao walio ngazi za juu watakuwa na tabia kama hii?

Sio tu ulafi wa mali na utawala ndio unaogandamiza Ummah wetu; bali pia kutotosheka na maisha. Kutotosheka huku kumeenea kwa sura ya ubinafsi na utaifa na kumetupa chaguo. Ikiwa naweza kuokoa siku yangu ya leo kupitia kuwauza ndugu zangu na dada zangu, basi hilo litakuwa ni chaguo sahihi.

Mtume wa Allah (saw) amesema:

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم «يوشك الأمم أن تداعى عليكم كما تداعى الأكلة إلى قصعتها فقال قائل ومن قلة نحن يومئذ قال بل أنتم يومئذ كثير ولكنكم غثاء كغثاء السيل ولينزعن الله من صدور عدوكم المهابة منكم وليقذفن الله في قلوبكم الوهن» فقال قائل يا رسول الله وما الوهن قال «حب الدنيا وكراهية الموت»

"…na Allah ataondoa vifuani mwa maadui zenu hofu kwenu na Allah atazigonga nyoyo zenu kwa al-Wahn" Mmoja akauliza, 'Ewe Mtume wa Allah, al-Wahn ni nini?' Akajibu, "Kupenda dunia na kuchukia kifo."

Mapenzi haya ya vitu vya kimada yaliyo penyezwa polepole yameuteka mujtamaa wetu. Tumegeuka kuwa watu tunaojali vitu na matabaka. Ulafi wa kufikia "kiwango cha juu" unawasukuwa watu kwenye haramu. Fesheni mpya ya gari kuwa nalo ni kitu cha lazima; najali nani ikiwa nitachukua mkopo wa riba benki almuradi niwe nalo. Matangazo ya kibiashara katika runinga yanaonesha kuwa mume atapewa kikombe cha chai ikiwa tu atakubali kuchukua mkopo kutoka benki ili mkewe aweze kurembesha nyumba yake. Hivi majuzi, mtindo mpya ulianzishwa nchini Pakistan kwa jina la sherehe ya harusi ya muda mrefu. Sherehe hii ya harusi iliendelea kwa muda wa mwaka mmoja na kusababisha shoo kufanywa kutokana nayo. Ukweli ni kuwa, hili, lilikuwa ni kuanzisha mtindo mpya wa kuonesha utajiri ambao hautachochea tu wivu bali pia ulafi kwa wengine kutaka zaidi, kwa njia yoyote iwayo.

Ni lazima tukumbuke kuwa kutotosheka ndiko kuliko wafanya Mayahudi kuchukiwa sana machoni mwa Allah kwani kuliwapelekea kumuasi Yeye (swt):

وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ النَّاسِ عَلَى حَيَاةٍ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُواْ يَوَدُّ أَحَدُهُمْ لَوْ يُعَمَّرُ أَلْفَ سَنَةٍ وَمَا هُوَ بِمُزَحْزِحِهِ مِنَ الْعَذَابِ أَن يُعَمَّرَ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ

"Na kwa hakika utawaona ni wenye pupa ya kuishi (Mayahudi), na kuliko washirikina. Kila mmoja wao anatamani lau angeli pewa umri wa miaka elfu. Wala hayo ya kuzidishiwa umri hayamuondoshei adhabu; na Allah anayaona wanayo yatenda. "[Al-Baqara: 96]

Sisi, kama Waislamu wa leo, ni lazima tuzingatie na kufahamu kuwa kadhia hii ya kinafsiyyah ya ulafi yaweza kutupelekea kumuasi Allah (swt) na yaweza kutupelekea kikamilifu katika upotevu kutokana na matamanio yetu. Hatuna budi kujifunza njia za kujitolea na ni lazima tuzungumzie juu ya haki zetu na za ndugu zetu ambazo zinapunjwa na watawala walafi walioko leo ili tufaulu hapa duniani na kesho akhera.

**Masoud Salim Mazrui**


Email: info@uqab.or.ke

# Ndoa Chini ya Mfumo wa Kisekula wa Kirasilimali ni Taasisi ya Ulimbikizaji Mali



**Habari:**

Mnamo Ijumaa, 11 Mei 2018, Mahakama ya Upeo ilikataa kubadilisha uamuzi wa kikao cha Mahakama ya Rufaa mjini Malindi wa mwaka 2015 kuwa mwanandoa anayestahiki ni sharti asimamiwe kwa kiwango cha maisha alichokuwa akiishi nacho kabla ya kuachana. Zaidi ya hayo, mnamo Jumatatu, 14 Mei 2018 Mahakama Kuu ilidumisha sheria ya Ndoa na Mali na hivyo basi wanandoa hawatahitajika kugawanya utajiri wao sawa kwa sawa wakati wa talaka. Katika uamuzi mkuu, Hakimu John Mativo alikataa ombi la Chama cha Mawakili Wanawake (FIDA) la kutaka kufutiliwa mbali sehemu ya 45 (3) ya sheria hiyo, inayosema kuwa wanandoa wanapasa kupata tu kile walicho changia katika utajiri wa familia.

**Maoni:**

Matukio mapya yanayo ibuka katika mahakama za Kenya ni tone katika bahari kuhusiana na majanga yanayoikabili taasisi ya ndoa chini ya mfumo batili wa kirasilimali. Chini ya usekula, dini haina mamlaka hivyo basi dola hutunga kanuni za mambo ya kibinadamu pasi na kuzingatia itikadi ya Muumba. Huku lengo pekee la dola likiwa ni kudhamini uhuru (uhuru wa kumiliki, uhuru wa kuabudu, uhuru wa kuzungumza na uhuru wa kibinafsi) ambazo zote zahitaji kufurahiwa na raia wake.

Nidhamu huru ya kijamii itokanayo na mfumo batili wa kisekula wa kirasilimali, huitazama taasisi ya ndoa kama muungano baina ya watu waliokubaliana kuishi kama wanandoa bila ya kujali jinsia zao, yaani, mwanamume aweza kumuoa mwanamume mwengine, mwanamke aweza kumuoa mwanamke mwengine, au mtoto aweza kumuoa mamake, au binti aweza kuolewa na babake nk. lengo la ndoa ni starehe za ngono na ulimbikizaji mali. Lengo limeamuliwa tokea mwanzo na lengo la maisha katika mfumo wa kisekula wa kirasilimali, ambalo ni kutafuta kiwango cha juu cha furaha kwa kushibisha viungo vya mwili. Hivyo basi, furaha imefungamanishwa na ulimbikizaji mali, ambao hatimaye hudhamini maisha ya hali ya juu.

Taasisi ya ndoa chini ya mfumo wa kisekula wa kirasilimali haizingatii mpangilio maalumu kabla ndoa. Zaidi, haijaweka wazi majukumu ya wanandoa kando na kuwa mmoja awe ni kifaa cha ngono na mwengine mnyanyasaji wa ngono. Kifaa cha ngono huingia katika muungano huu kwa malengo ya kulimbikiza mali, huku mnyanyasaji wa ngono anataka kujitukuza kibinafsi kwa jina la utafutaji furaha. Taasisi hii imejaa vurugu kiasi ya kuwa utulivu haupatikani badala yake fujo na uhasama ni mambo ya kila siku yanayo wakabili wanandoa. Maisha ya fujo ya wanandoa yameghubikwa na maisha ya kujifanya kuwa kila kitu kiko sawa!

Uamuzi huo wa mahakama unatudhibitishi hakika mfumo wa kisekula wa urasilimali umefeli pakubwa katika kusimamia mambo ya wanadamu hivyo basi ni lazima ubadilishwe kwa mfumo safi wa Kiislamu wenye kutekelezwa kikamilifu chini ya Khilafah (Dola ya Kiislamu) yenye kusimamishwa tena kupitia njia ya Mtume (saw).

Nidhamu ya Kijamii ya Kiislamu inatambua kwamba panapo kuwa na mwanamume na mwanamke ni lazima pawe na uhusiano na udhibiti ni lazima uuzunguke uhusiano huo. Uhusiano huu ni lazima ujengwe kwa msingi wa ndoa. Lengo la ndoa ni kutafuta radhi za

*Endelea Uk..8*

Allah (swt) kupitia kuendeleza kizazi kama ilivyo pitishwa na Allah (swt) na kufikia lengo hili; wanandoa wanahitaji kuoana kupitia mkataba sahihi wa ndoa unaowaunganisha kama wandani na watumwa wa Allah (swt) watakaoishi kwa utulivu.

Katika Uislamu, ndoa ni baina ya mwanamume Muislamu na mwanamke/wanawake (2/3/4) au mwanamke/ wanawake (2/3/4) watu wa kitabu (ahlu al-Kitab). Mume wa kuzingatiwa ni lazima awe angaa mwenye tabia nzuri na kujitolea katika njia ya Allah (swt). Huku mke/wake (2/3/4) wa kuzingatiwa ni sharti wafuzu kuolewa na ni lazima wawe angaa mke/wake (2/3/4) wenye tabia nzuri na kujitolea katika njia ya Allah (swt).

Katika Uislamu mume, na mke/wake (2/3/4) wana majukumu waziwazi ambapo mume anapaswa kusimamia mambo nje ya nyumba na mke/wake (2/3/4) wanapaswa kushughulikia mambo ya ndani ya nyumba. Kuishi pamoja kwa wanandoa kumejengwa juu ya usuhuba kwa msingi wa kipimo cha halal na haram. Wote wakiogopa siku ya akhera ambayo watahisabiwa juu ya majukumu yao katika ndoa. Kila mmoja kati ya wanandoa hawa anahusika na udumishaji ndoa hii na ikiwa wanandoa hawa watajiona kutowiana katika upande wa kuwa na mtazamo mmoja, wa kutafuta radhi za Allah (swt) basi wanaruhusiwa kutalikiana kwa utu na kwa njia ya uchaMungu.

Kwa ufafanuzi mfupi huu wa nidhamu ya kijamii ya Kiislamu, unathibitisha kuwa pindi Uislamu utakapo tekelezwa kikamilifu chini ya Khilafah (Dola ya Kiislamu) itakayo simamishwa tena kwa njia ya Mtume (saw), utadhamini utulivu, furaha na ufanisi katika taasisi ya ndoa na nyanja zote za maisha. Kinyume na hali iliyoko sasa ya mateso na uzorotaji wa watu ambao umekuwa duni zaidi ya mnyama chini ya mfumo huu mchafu na batili wa kisekula wa kirasilimali ambao umewafanya watu kuwaabudu watu wengine badala ya Muumba wao kwa sababu ya hamu yao ya kulimbikiza au kushibisha kiu yao ya mali.

Mwamko wa Kenya na Afrika kwa jumla uko katika kuukumbatia mradi wa Khilafah. Kwa kubadilisha mfumo wa kisekula wa kikoloni wa kimagharibi wa kirasilimali, ambao ndio shina la mateso na majanga ya bara hili pamoja na ulimwengu, yanayoshuhudiwa leo!

**Ali Nasoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

*Endelea Uk..8*

# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 13: Mivutano ya Kifikra na Mapambano ya Kisiasa Walioyafanya Maswahaba (ra)



Katika Halaqa hii tutaangalia mvutano wa kifikra na mapambano ya kisiasa walioyafanya maswahaba (ra).

Msimamo wa maswahaba (ra) ulikuwa imara pasi na kuyumba katika kupambana na kila yanayokhalifu Uislamu na kuyakabili ili kubainisha uongo wake. Hawakujali yatakayotokea wala hali itakavyokuwa katika kushikamana kwao na mfumo (Uislamu) pekee, pasi na kuingiza mahisabu yoyote ila mfumo (Uislamu). Wakimtegemea Allah juu ya hilo, Wakiamini nusra kutoka kwake, wakimuamini kwa imani ya hali ya juu...!

Na ili kuyabainisha hayo tutataja mwenendo mmoja na kugusia msimamo katika misimamo ya kimfumo waliosimama kwayo maswahaba (ra) wakiwa wamezama katika mvutano wa kifikra na mapambano ya kisiasa...!

Huu msimamo ni kwa njia ya mfano tu wala sio kutaja misimamo yote ya maswahaba (ra), kwani misimamo yao ya kimfumo ni mingi Haiwezi kuhifadhika, wala hayatoshei Maqam haya kuyataja, kuitaja inahitaji msururu wa vitabu/mijeledi...!

**Msimamo wa swahaba Uthman Ibnu Madh'un (ra) katika kuvumilia shida na maudhi katika Njia ya Allah:**

Amepokea Abu Nuaym katika hulya kutoka kwa Uthman asema: Alipoona Uthman Ibnu Madh'un (ra) yanayowapata maswahaba (ra) wa Mtume (saw) kutokana na mitihani naye anatembea kwa amani ya Walid bin Mughera, alisema: "Wallahi hakika kutembea kwangu kwa amani katika hifadhi ya mtu mshirikina, na wenzangu watu wa dini yangu wanapata mitihani na maudhia katika njia ya Allah nami hayanipati, ni upungufu mkubwa katika nafsi yangu! Akamwendea Walid bin Mughera akamwambia: "Ewe Aba Abdi Shams! Umetekeleza dhima yako, nimekurudishia hifadhi yako!" Akasema: "Kwa nini ewe mtoto wa ndugu yangu?! Huenda kuna mtu amekuudhi katika jamaa zangu?" Akasema: "La, lakini mie naridhia hifadhi ya Allah azza wa jalla, wala sitaki hifadhi ya mwengine asokuwa

*Endelea Uk..10*

yeye...! Akasema: “Twende msikitini, unirudishie hifadhi yangu waziwazi, kama nilivyo kuomba hifadhi waziwazi”. Asema: Wakaondoka mpaka walipofika msikitini, akasema Walid bin Mughera: “Huyu hapa Uthman, amekuja kunirudishia hifadhi yangu, akasema Uthman (ra): “Amesema kweli, Nimependa nisiwe na hifadhi isiokuwa ya Allah, nimeshamrudishia hifadhi yake!”

Kisha akaondoka Uthman (ra), na mshairi Labid bin Rabia’h yuko katika mkao wa Maqureysh anawaimbia. Uthman akaketi nao, akasema Labid: “Jueni na mtambue kila kinachoabudiwa asokuwa Allah Ni batil”. Akasema Uthman: “Swadaqta”. Akasema Labid: “Na kila neema lazima zitaondoka” Akasema Uthman: “Umesema uongo Hakika Neema ya watu wa Jannah itabakia”. Akasema Labid bin Rabia’h: “Enyi mkusanyiko wa Maqureysh, Wallahi hiki kikao chenu hakikuwa na maudhi! Haya yamezuka lini?” Akasema mmoja katika Jamaa: “Hakika huyu ni safihi ana wenzake masafihi, walioacha dini yetu, usipate tabu na maneno yake”. Uthman akamrudishia majibu mpaka maneno yakawa makubwa kati yao. Yule bwana akamwenukia akamtia kofi Uthman mpaka macho yakabadilika rangi kwa kipigo kizito. Na Walid bin Mughera yupo karibu anaona yaliomfika Uthman. Akasema Walid: “Ama Wallahi ewe kijana cha ndugu yangu! Jicho lako lilikuwa na hifadhi kwa yalolipata, ulikuwa katika hifadhi nzuri”, akasema Uthman: “Bali Wallahi! Hakika hili jicho langu zima lahitaji haya yaliolipata hili mwenzake! Na mimi niko katika hifadhi ya Mwenyezi Nguvu na uweza zaidi ewe Aba Abdi Shams!” Kisha akasema Walid: “Njoo ewe mtoto wa ndugu yangu urudi katika hifadhi yako”, Akasema: “Laa”

Na Uthman Ibnu Madh’un (ra) alikuwa ni mshairi akasema kwa yale yaliolipata jicho lake:

Ikiwa jicho langu liko katika radhi za Allah linapatwa na mkono,

Wa anaepinga dini ambaye sie muongofu,

Basi Rahmani amenipa badali yake thawabu,

Na yule aliyeridhiwa na Rahmani enyi jamaa zangu atapata Raha,

Hakika yangu mimi hata mkisema amepotea mjinga yuko katika dini ya Mtume (saw)

Namtaka kwa hilo Allah na haki ni dini yetu

Kusudi kwa atakaye vuka mipaka na kutufanyia uadui

**Itaendelea katika UQAB Toleo 18…In Shaa Allah.**

# SWALI/JAWABU:
# Ziara ya Mohammad Bin Salman ya Uingereza, Amerika na Ufaransa




**Swali:** Mfalme Mtarajiwa wa Saudia, Mohammad Bin Salman, alikamilisha ziara yake nchini Ufaransa, iliyo anza mnamo Jumatatu 09/04/2018 na kuchukua siku mbili hadi 10/04/2018. Awali alizuru Uingereza mnamo 10/03/2018 kwa siku tatu. Ikufiatiwa na ziara ya Amerika, kuanzia 20/03/2018 hadi 08/04/2018 … alipokewa kama kiongozi wa dola. Hivyo basi ni kipi kilicho nyuma ya ziara hizi? Jambo ambalo si la kawaida ni kuwa ziara hizi ni kwenda kwa wahusika wenye maslahi tofauti; ni kipi kilicho sawia baina yao? Tafadhali fafanua jambo hili, na Allah akulipe kheri.

**Jibu:** Ziara kuu ya Mohammad Bin Salman (MBS) ni ile ya kwenda Amerika. Ziara yake ya Uingereza ni ziara ya maliwazo, kwa sababu alichukua hatua kali dhidi ya vibaraka wake nchini Saudi Arabia. Ziara yake nchini Ufaransa ni ziara ya pembeni ya kujenga mazingira ya umaarufu kwake, ili isemekane kuwa Bin Salman alizuru nchi kuu barani Amerika na Ulaya; haya hapa ni maelezo yake:

**Kwanza: Ziara ya Mohammad Bin Salman kwenda Uingereza:**

Ziara ya Mohammad Bin Salman kwenda Uingereza ilianza mnamo 07/03/2018 na kuchukua siku tatu hadi 10/03/2018. Kama tulivyo taja mwanzoni, ilikuwa ni ziara ya kuiliwaza Uingereza, kwa sababu MBS anajua kwamba Uingereza ina mizizi thabiti katika familia ya kifalme ya Saudi na hivyo basi yaweza kumletea yeye matatizo. Na hivyo basi aliizuru Uingereza kujenga mazingira ya utulivu kwa kufunga nayo mikataba ya kiuchumi ingawa haikuwa nyingi.

Hili lilithibitishwa katika taarifa ya mwisho. Ilikuwa karibu na ziara ya kawaida ikiwa na makubaliano ya kawaida kwa maneno jumla yasiyo na ufafanuzi, isipokuwa katika baadhi ya ofa za kiuchumi. Kwa mfano, taarifa hiyo ya mwisho ilieleza:

Uingereza inathibitisha usaidizi wake imara kwa ruwaza ya Saudia ya 2030 na mpango wa kiuchumi na kijamii wa Ufalme wa Saudi Arabia unaolenga upanuzi wa uchumi.

- Mwana wa kifalme Mohammad Bin Salman na Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, mnamo Jumatano walizindua Baraza la kila mwaka la Ushirikiano wa Kimikakati kama hatua muhimu ya kuwepo kwa mzungumzo ya mara kwa mara kuimarisha nyanja zote za ushirikiano kati ya nchi mbili hizi …. Saudi Arabia inasifu ujuzi na tajriba ya Uingereza katika sekta mbali mbali za elimu kuanzia elimu ya chekechea, msingi na sekondari mpaka elimu ya juu na mafanikio katika mafunzo ya kiufundi … Saudi Arabia inafahamu ujuzi

Endelea Uk..12

wa Uingereza katika matibabu … Uingereza imesifu umuhimu wa kuorodheshwa kwa mafanikio kwa kampuni ya Aramco katika soko la hisa kama sehemu ya mpango wa marekebisho ya kiuchumi ya Ufalme wa Saudi Arabia … na Saudi Arabia imeunga mkono msimamo wa London kama kituo kikuu cha kifedha duniani …

Soko la Hisa la London limekubaliana pamoja na Soko la Hisa la Saudia (Tadawul) juu ya mpango wa kujenga uwezo na mafunzo ili kusaidia kuimarisha masoko ya hisa. Saudi Arabia na Uingereza zimesisitiza umuhimu wa mahusiano ya kiulinzi na kiusalama na dori yao katika kupata kwa pamoja utulivu wa kiusalama na wa kieneo. Nchi mbili hizi zilitangaza nia zao za kuangazia juhudi za kupambana na ugaidi na misimamo mikali kwa kubadilishana habari na kufahamu njia ambazo magaidi na wenye misimamo mikali huzitumia kuyashawishi makundi dhaifu. Nchi mbili hizi zimetia saini maelewano kadhaa ya pamoja kumakinisha zaidi ushirikiano na ushirika baina yao. Pia inajumuisha kutia saini maelewano yenye nia ya kutangaza hamu ya pande hizo mbili ya kukamilisha mazungumzo baina yao ili kufikia makubaliano ya Ufalme huo kupokea ndege 48 ziada za kivita aina ya Typhoon. Nchi mbili hizi pia zilisisitiza haja ya Iran kujifunga na misingi wa ujirani mwema na kutoingilia kati mambo ya kindani ya nchi hizo.

B) Baadhi ya mambo jumla ya kisiasa na ya kiusalama, ambayo hayakuangaziwa au kufafanuliwa kwa suluhisho la kina katika kadhia:

- Nchi mbili hizi zilisisitiza umuhimu wa kufikia suluhisho la kisiasa kwa mgogoro nchini Yemen kwa msingi wa mpango wa GCC na hatua za utabikishwaji wake, na matokeo ya mazungumzo ya kitaifa ya Yemen na azimio la Baraza la Usalama la 2216, ambalo litapelekea kupatikana kwa suluhisho la kisiasa litakalo dhamini usalama wa Yemen na hadhi ya eneo lake. Pande mbili hizi zilidhihirisha uungaji mkono wake imara kwa mjumbe mpya maalumu wa Umoja wa Mataifa (UM) aliyeteuliwa kwa ajili ya Yemen, Martin Griffith … Walikubaliana juu ya umuhimu wa jamii ya kimataifa kushinikiza wanamgambo Mahouthi ili kuruhusu utoaji msaada wa kibinadamu usio na pingamizi … Uingereza iliipongeza Saudi Arabia kwa kuendelea kujitolea ili kuhakikisha kampeni hiyo ya muungano wa majeshi iko sambamba na kanuni ya kimataifa ya kibinadamu … nchi mbili hizo zilithibitisha upya kujitolea kwao kwa suluhisho la kuwepo nchi mbili, kwa msingi wa Mpango wa Amani wa Waarabu na maazimio muwafaka ya UM.

C) Baadhi ya mikataba ya kiuchumi yenye nia ya kuliwaza, kama natija ya matendo ya Bin Salman dhidi ya vibaraka wa Uingereza:

- Saudi Arabia na Uingereza zimejitolea katika ushirikiano wa muda mrefu kusaidia kupatikana kwa Ruwaza ya 2030, ili kujumuisha sekta nyingi, ikiwemo: kutathmini fursa za uwekezaji wa pamoja na Uingereza (na kupitia) Hazina ya Uwekezaji wa Ummah na biashara ya pamoja kati ya nchi mbili hizi…fursa hizi kwa pamoja zitagharimu dolari bilioni 100 kwa zaidi ya miaka 10, ikiwemo Hazina ya Uwekezaji wa Ummah (PIF) huku uwekezaji wa moja kwa moja ukigharimu dolari bilioni 30.

- Uingereza na Saudi Arabia zimekaribisha mikataba kadhaa mikubwa ya kibiashara waliyokubaliana pamoja wakati wa ziara hiyo; zinatarajiwa kuzidi dolari bilioni 2, kuunda na kudhamini nafasi za kazi na ufanisi nchini Saudi Arabia na Uingereza.

Ni wazi kutokana na hili kuwa ziara hiyo haiendi zaidi ya lengo lake, ambalo ni kuliwaza na kutuliza, takriban ziara yote ilikuwa ubadilishanaji jumla wa maneno, isipokuwa katika baadhi tu ya ahadi za kiuchumi, ambazo si muhimu na wala hazina uzito.

**Pili: Ziara ya Mohammad Bin Salman kwenda Amerika:**

Mfuatiliziaji wa ziara ya MBS kwenda Amerika ataona kuwa Amerika inamuunda MBS kuwa mtumwa mtiifu kwake; inamdhalilisha mbele ya uso wake naye anatabasamu na inamtishia naye anajisalimisha; huu hapa ufafanuzi wake:

1) Baada ya kuchukua utawala baada ya kifo cha kakake, Abdullah, mnamo 23/1/2015, Mfalme Salman alianza mipangilio ya haraka ya kumakinisha utawala wake na wale watakao kuja baada yake. Alimng'oa kakake, Muqrin bin Abdulaziz kutoka katika cheo cha Mfalme Mtarajiwa, ambaye ni mtiifu kwa Uingereza, na kumteua mwanawe Mohammad Bin Salman (MBS) kama Mfalme Mtarajiwa, na kumkabidhi nguvu nyingi za kuimarisha utawala wake. Aliwang'oa na kuwatenga wengi wa wapinzani wake na wale ambao ni vibaraka wa Uingereza katika familia yake, na kuonesha utiifu wake mkubwa kwa Amerika. Hatua ya pili ilikuwa ni kuwafanya Waamerika kuwa karibu zaidi na MBS na uwezo wake, ili kumfahamu vizuri na kupima utiifu wake kwa Amerika. Hivyo basi alizuru Washington mnamo 15/3/17 baada ya kutawazwa rasmi kwa Trump kama Raisi wa Amerika, na Trump alimpokea kwa daraja ya juu katika ikulu ya White House mbele ya makamu wake wa raisi, Pence, na usalama wake wa taifa wa Amerika, akinyanyua daraja ya ziara hiyo. Trump alionesha uungaji mkono wake kwa Bin Salman. Hatua nyengine ilijiri mnamo 4/11/2017 ili kuimarisha mamlaka ya MBS kwa kukata mbawa za vibaraka wa Uingereza na wengineo na kumueka kila mmoja ndani ya udhibiti wake, na kuwadhalilisha na kutishia kufunga akaunti zao, ambapo mamia ya wana wafalme, mawaziri, ma-afisa na wafanyi biashara waliwekwa kizuizini kwa kisingizio cha kupigana na ufisadi. Alitangaza kuwa alikusanya kutoka kwao dolari bilioni 100.

Na hivi sasa, inakuja hatua nyengine kabla ya mwisho; ziara yake kwenda Washington kwa mara ya pili ili

*Endelea Uk..13*

kuimarisha utiifu wake kwa Amerika na kuimarisha mafungamano yake kwake na kufanya matayarisho kwa hatua ya mwisho, kuteuliwa kwake kama mfalme halisi katika wakati wanaotarajia hivi karibuni. Pindi Bin Salman alipoanza ziara zake za kigeni, alipokewa kama mfalme, kama ilivyo tokea nchini Misri mnamo 4/3/2018, na ziara yake ya Uingereza mnamo 7/3/2018 ambapo alipokewa na Malkia, na kisha kufuatiwa na mapokezi na ziara ndefu nchini Amerika zinazo thibitisha hili. Trump alitaja hili alipozungumza na Bin Salman: “Kumekuweko na mambo mazuri tangu ziara yako ya mwisho ikuluni White House. Wewe ndiye mfalme mtarajiwa” wakati wa ziara yako ya mwisho, alisema, “na sasa wewe ni zaidi ya mfalme mtarajiwa.” (Chanzo: Russian Sputik 21/3/2018)

2) Kwa hivyo punde tu Bin Salman alipofika Washington, alikutana na Raisi Trump mnamo 20/3/2018 M. Trump alisema: “Ni heshima kubwa kuwepo na Mfalme Mtarajiwa pamoja nasi, Saudi Arabia imekuwa rafiki mkubwa … Nilikuwa nchini Saudi Arabia mnamo Mei. Na tunaziregesha bilioni za dolari nchini Amerika … Na kitu chengine ambacho ninafuraha nacho zaidi ni kuwa tulizungumzia kuhusu uwekezaji ulio na thamani ya dolari bilioni 400,” Aliendelea: “Tunafahamiana. Saudi Arabia ni taifa tajiri mno, na twatarajia wataipa Amerika baadhi ya utajiri huo, kwa njia ya ajira, kwa njia ya ununuzi wa vifaa bora vya kijeshi duniani kote.”

Bin Salman alijibu: “mahusiano kati ya Saudi Arabia na Amerika, ni mahusiano ya jadi … zaidi ya miaka 80 ya muungano na maslahi makubwa – kisiasa, kiuchumi, na kiusalama, katika kila eneo – maeneo mengi … Na msingi wa uhusiano huo, ni mkubwa sana na wenye kina kikuu … tulipanga kutumia dolari bilioni 200 kwa ajili ya fursa za miaka minne ijayo, lakini ikaishilia kuwa dolari bilioni 400 kwa ajili ya fursa hizo”. (Chanzo: CNN 20/3/2018).

Amerika inaitishia Saudi Arabia na kufuja mali ya Waislamu kupitia watawala hao waliokhini amana na kuukhini Ummah. Anachojali Trump na Waamerika ni kufyonza pesa za Waislamu kupitia familia ya Saud, waliotangaza utiifu wao na muungano wao kwa makafiri, na kuwahudumia kwa kulinda maslahi yao eneo la Mashariki ya Kati, na kwa kufadhili uchumi wao na kulipa gharama zote za kulinda maslahi yao.

3) Trump alionesha karata zake mbele ya kamera na kuziweka dhidi ya kifua cha Bin Salman kwa michoro na picha za silaha ambazo Saudi Arabia itazinunua kutoka Amerika na itazipokea hivi karibuni. Alizihesabu dili na aina za silaha zenye thamani ya mabilioni, akimwambia kuwa: “Hiyo ni kidogo sana kwako.” Trump alisema: “Dili hizi zitazalisha nafasi mpya za kazi (nchini Amerika) na zinatarajiwa kufikia nafasi za kazi elfu 40.” (Chanzo: Sputnik Russian 21/3/2018). Kinacho bakia ni kuwa Trump anaweka kamba katika karata hizo na kuifunga shingoni mwa Bin Salman kana kwamba anamtumia ujumbe kuwa usaidizi wetu kwako ni kwa badili kiwango gani cha pesa utakazo tupa, na kuitoa ardhi kwa matumizi yetu, na kufanya kila kitu tunacho agiza bila ya pingamizi yoyote. Kitendo hiki kilikuwa ni tusi kwa Bin Salman aliyejibu kwa tabasamu kama bwege huku Trump akionesha jeuri na kutojali.

4) Wakati wa ziara ya MBS, alikutana na maafisa katika idara hiyo na sekta nyenginezo muhimu:

A) Alikutana na Waziri wa Ulinzi wa Amerika, Mattis, na Mkuu wa Majeshi, Danford, akithibitisha utiifu wake kwa Amerika: “Changamoto za leo sio za kwanza ambazo nchi mbili hizi zimekabiliana nazo. Leo tunakabiliana na changamoto kali zaidi eneo hili na ulimwenguni, ima kutokana na vitendo vya serikali ya Iran au changamoto za makundi ya kigaidi,” alisema. (Chanzo: Gazeti la Saudia la Al-Wi’am 24/3/2018). “Ni lazima pia tuimarishe juhudi za haraka za kutafuta azimio la amani la vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Yemen na tunakuunga mkono kwa hili.”, “Waziri wa Ulinzi wa Amerika, Mattis, alimwambia Mfalme Mtarajiwa Mohammad Bin Salman. “Tutavimaliza vita hivi na kwa njia nzuri kwa watu wa Yemen, hii ni kwa uchache”, pia aliahidi kufanya kazi na Riyadh kuimarisha “utulivu na usalama” eneo hili (Chanzo: Reuters, 22/3/2018). Kadhia ya Yemen ni kadhia ambayo Amerika bado haijafanikiwa kupata malengo yake ya mwisho, na Saudi Arabia, ambayo inafanya kazi hiyo ya kufanikisha kupatikana kwa malengo ya Amerika, bado iko katika mgogoro na bado haijaweza kujitoa ndani yake. Mwisho wa kadhia hii na kujiondoa salama kwa Saudi Arabia kutaimarisha mamlaka ya Bin Salman.

- Bin Salman alitoa taarifa kwa jarida la Time mnamo 31/3/2018 ambapo alisema: “Tunaamini vikosi vya Amerika ni sharti vibakie kwa muda wa angaa nusu muhula, ikiwa si kwa muda mrefu … Amerika inahitaji kuwa na karata za kujadiliana na kutia shinikizo. Ukivitoa vikosi hivi nje, utapoteza karata hii” … “Bashar anabakia”, alisema. “Lakini naamini kuwa maslahi ya Bashar sio kuwaruhusu Wairan kufanya chochote wanachotaka kufanya.” Raisi wa Amerika Trump alisema mnamo Jumanne 3/4/2018: “Nataka kutoka (nchini Syria). Nataka kuviregesha vikosi nyumbani. Nataka kuanza kujenga upya taifa letu.”

“Kuhusiana na Syria, kazi yetu msingi ilikuwa ni kuiangamiza ISIS. Tunakaribia kukamilisha kazi hiyo. Na tutafanya uamuzi kwa haraka kwa ushirikiano na wengine katika eneo hili wa kipi tutakacho fanya. Saudi Arabia inahamu ya uamuzi wetu. Na nimesema, wajua, munataka sisi tubakie, na huenda mukalipia hilo.” (Chanzo: AFP, 3/4/2018). Hivyo, Trump anaendeleza sera ya vitisho kwa serikali ya Al Saud, ambayo inaumakini wa kudumisha ushawishi wa Amerika eneo hilo.

Pia alitoa taarifa kwa jarida la Atlantic mnamo 2/4/2018 alipoulizwa: “Je, unadhani Mayahudi wana haki ya kuwa

*Endelea Uk..14*

na taifa angaa katika baadhi ya sehemu za ardhi ya mababu zao?" alisema:

"Naamini kuwa kila mtu, popote pale, ana haki ya kuishi katika taifa lao la amani … Naamini Wapalestina na Waisraeli wana haki ya kuwa na ardhi zao wenyewe." (Chanzo: Tovuti ya Kisaudi ya Al Wi'am 3/4/2018)

Bin Salman hakuficha khiyana yake hata dhidi ya Ardhi Tukufu, ardhi ya Isra na Miraj.

- Na kwa jina la burudani, aliweka bajeti kubwa. Mwenyekiti wa Mamlaka Jumla ya Burudani nchini Saudi Arabia, Ahmed Bin Aqeel Al Khatib, alitangaza "nia ya mamlaka hiyo ya kuwekeza mpaka riyal bilioni 240, sawia na dolari bilioni 64 katika sekta ya burudani kwa miaka kumi ijayo." Na kutangaza kujengwa kwa Jumba la Opera, la kwanza tangu kubuniwa kwa Ufalme huo" (Chanzo: Tovuti ya Al Arabiya 22/2/2018).

- Gazeti la Washington Post, mnamo siku ya nne na ya mwisho ya ziara yake jijini Washington na mkutano na maafisa wake mnamo 24/3/2018, lilifanya mahojiano na Bin Salman aliyesema, "Wakati wa mkutano huo, vita nchini Yemen, mpangilio wa amani wa Mashariki ya Kati, Iran, mpangilio wa mageuzi wa kindani, na matarajio ya Saudia ya nuclear yalizungumzwa." Alisema kazi yake kubwa nchini Amerika ni kujishindia imani ya wawekezaji wa Amerika ikiongezewa na kupata usaidizi wa kiteknolojia na wa kielimu ili kusaidia juhudi za mageuzi nchini Saudi Arabia. Alisema kwa kadhia za magazeti kuhusu kuwapa wanawake nyingi ya haki zao … Hii yamaanisha kuwa faili za eneo zima zilifunguliwa mbele yake na kuzungumzwa pamoja naye. Kwa hivyo anajua namna ya kuyatekeleza na kukimbilia usaidizi wake na utekelezwaji wake na Waamerika. Sehemu ya swali la Yemen, kuna mpango wa Trump katika Mashariki ya Kati na suluhisho kwa suala la Palestina; yeye (Trump) alisema kuwa atatangaza mpango katika miezi ijayo baada ya kuitambua Jerusalem kama makao makuu ya umbile la Kiyahudi ambalo yeye (Bin Salman) atafanya maridhiano nalo, pamoja na kubadilisha sera ya ndani ya Saudia kwa kile Amerika inachotaka; ili kuifanya nchi hiyo kuwa ya kisekula na kupenyeza maadili ya hadhara ya Kimagharibi ndani yake, pamoja na kuwapa wawekezaji wa Kiamerika fursa za kuudhibiti kikamilifu uchumi wa nchi hiyo.

Tovuti ya Arabic 21, mnamo 29/3/2018, ilinukuu gazeti la Kiingereza la The Independent likisema kwamba limeona mpango wa Mfalme Mtarajiwa wa Saudia, Mohammad bin Salman, ambao unajumuisha mikutano ya wakuu wa makampuni makubwa, wanasiasa, wenye mafuta, na wafanyi kazi katika teknolojia, burudani na sanaa unalenga kushikilia kandarasi kwa rai jumla ya Kiamerika. Kituo cha habari cha CBS kilifanya mahojiano naye katika kipindi "Sixty Minutes", mahojiano ya kwanza ya kituo hicho kuwahi kumfanyia kiongozi wa Kisaudi kwa miongo kadhaa. Alitumia fursa hii kuboresha sura yake kama mwanamageuzi mchanga mkakamavu anaye tekeleza mageuzi muhimu, kama vile kudhibiti mamlaka ya polisi wa kidini na kuruhusu wanawake kuendesha magari. Gazeti hilo lilitaja kuwa alikutana na maafisa wa zamani mnamo Jumanne (27/3/2018) kama Kissinger, Bill Clinton na Hillary Clinton na wengineo, na wamiliki wa mageti makubwa, na atakutana na Raisi wa zamani Obama, na Waziri wa Kigeni wa zamani John Kerry, na David Petraeus.

**- Bin Salman alionesha kujisalimisha zaidi na unyenyekevu zaidi alipotuma, baada ya kuondoka Amerika na kuelekea Ufaransa, ujumbe wa utiifu kwa Trump wa Amerika, ambao alisema: "Mheshimiwa, Raisi Donald Trump wa Amerika, salamu: Nina furaha wakati ninapo ondoka nchi yako, mshirika wetu, kudhihirisha shukrani zangu kwako kwa ukarimu wako kwangu na wajumbe nilio andamana nao, na kuchukua fursa hii kutoa heshima zangu kwa mara nyengine tena kwa mahusiano ya kihistoria na kistratejia baina ya nchi zetu mbili, ambazo zinashuhudia maendeleo zaidi katika nyanja zote, na siwezi kukosa kusisitiza kuwa mazungumzo yaliyo fanyika wakati wa ziara hii yatachangia katika kumakinisha zaidi mahusiano haya na kuyaimarisha, na kuimarisha mafungamano ya ushirikiano wa pamoja … nakutakia afya njema na furaha, na kwa watu wa Amerika kudumu na maendeleo na ufanisi"**

**Tunatamatisha kuzungumzia ziara hii kwa kurudia yale tuliyo yasema mwanzoni. (Mfuatiliziaji wa ziara ya Bin Salman kwenda Amerika ataona kuwa Amerika inamuunda Bin Salman kama mtumwa wake mtiifu; inamdhalilisha mbele ya uso wake na huku anatabasamu na kumtishia na huku anajisalimisha).**

**Tatu: Ziara ya Mohammad Bin Salman kwenda Ufaransa:**

1) Ziara hii ya Bin Salman kwenda Ufaransa ni ziara ya mapito pembeni kujenga mazingira ya umaarufu kwa Bin Salman, ili isemekane kuwa alizuru Magharibi, kuanzia Uingereza mpaka Amerika na kisha Muungano wa Ulaya (Ufaransa). Na kwa sababu ya kukosekana umuhimu wa ziara hii, imekosa hata mpangilio wa kidiplomasia wa ziara za kimataifa. Kwa mfano, "Afisa katika afisi ya waziri mkuu wa Ufaransa alisema mnamo Jumatatu kwamba Mfalme Mtarajiwa wa Saudia alifutilia mbali ziara yake katika jumuiko kubwa la kampuni zinazoibuka za teknolojia jijini Paris kuangazia kina cha mahusiano ya kiteknolojia kati ya Ufaransa na Saudia. Kwa mujibu wa gazeti la LA Tribune: kufutiliwa huko kwa ziara ya mwana wa mfalme Mohammad kwa kituo cha "Station F" huenda ikamuacha Macron kuhisi bugudha, hususan kwa kuwa katika ziara ya Bin Salman kwa magwiji wa teknolojia katika Bonde la Silicon nchini Amerika wiki iliyo pita, Bin Salman aliweka sharti la kuzuru kawanda hili lililo amsha hasira za Macron …".

*Endelea Uk..15*

Mtandao wa Arab World mnamo 09/04/2018, ukinukuu (© REUTERS / POOL) uliripoti:

LA Tribune lilifichua kuwa Mfalme Mtarajiwa wa Saudia Bin Salman amemkasirisha Raisi wa Ufaransa Emmanuel Macron kwa kuweka sharti kwa kampuni za Kifaransa kunufaika kutokana na kandarasi za kibiashara na Ufalme huo, gazeti hilo lilisema. "Bin Salman alimueleza Macron kuwa kampuni za Kifaransa, kama vile kampuni za Kiamerika, huenda zikanufaika kutokana na kandarasi za Ufalme huo, maadamu tu hazitafanya biashara na Iran, likiongeza kuwa sharti hili liliamsha hasira za Macron".

2) Na kile walichokuwa "wakiringia" kuhusu kandarasi ya ushirika wa kistratejia haikutiwa saini, lakini wakaakhirisha saini hiyo kwa miezi minane hadi mwisho wa mwaka wa 2018.

Inajulikana kuwa mabadiliko katika sera ya kimataifa huwa ya haraka. Hivyo basi, ahadi za kutia saini makubaliano hayo au kukamilishwa kwa kandarasi hizo aghalabu hazitimizwi hususan ikiwa makataa ni marefu. Duru za karibu na afisi ya Raisi wa Ufaransa zimewatangazia maripota kuwa Macron na Mohammad Bin Salman watatayarisha hati ya kistratejia ambayo itakuwa tayari mwishoni mwa mwaka huu. Hii itapelekea kuwepo kwa kandarasi ambazo zitapelekwa (na Macron) Saudi Arabia mwishoni mwa mwaka huu kwenda kutiwa saini (Chanzo: Al Bayan 10/4/2018). Mtandao wa Al Arabiya pia uliripoti mnamo Jumatatu 9/4/2018: "Raisi na mwana wa mfalme watafanya kazi pamoja juu ya hati ya kistratejia ambayo itakuwa tayari kufikia mwishoni mwa mwaka huu na kuzalisha kandarasi zitakazotiwa saini pindi Macron atakapo kwenda Saudi Arabia kabla ya mwisho wa mwaka huu," haya pia yaliripotiwa na shirika la habari la France 24, mnamo 09/04/2018.

3) Zaidi ya hayo yale ambayo Raisi wa Ufaransa ametangaza yamo ndani ya muundo wa matarajio na chini ya mipangilio inayo hitaji kujadiliwa na kushauriwa ili kandarasi hizo ziwe barabara:

"Tunatarajia ushirikiano mpya, unao angazia kwa uchache kandarasi za sasa na zaidi uwekezaji kwa ajili ya mustakbali, hususan katika nyanja za dijitali na kawi," afisi ya Raisi wa Ufaransa imesema. (Chanzo: AFP 05/04/2018)

Ziara ya Muhammad Bin Salman nchini Ufaransa inatarajiwa kutamatisha kutiwa saini kwa baadhi ya makubaliano ya mikataba katika nyanja tofauti tofauti, kama vile utalii, ambapo Paris itaisaidia Riyadh kuangazia eneo la Al Hijr (Mada'in Salih) iliyo orodheshwa na shirika la UNESCO kuwa Turathi ya Kiulimwengu katika eneo la kaskazini magharibi mwa Ufalme huo pamoja na nyanja nyenginezo kama afya, kawi, uchukuzi, nk. (Chanzo: AFP, 08/04/2018)

4) Hivyo basi, hakuna kandarasi za maana za kiuchumi zilizotiwa saini katika ziara hii, kwa sababu ilikuwa ni ziara fupi (siku mbili), iliyo sababisha fedheha kwa Kasri la Elysee. Hii ndio sababu jibu la swali kuhusu ziara fupi ya mwana wa mfalme wa Saudia nchini Ufaransa baada ya ziara ya wiki tatu nchini Amerika, lili eleza: Kasri la Elysee linakaribisha kujumuishwa kwa Ufaransa kama mojawapo ya ziara za kwanza za kigeni za Mfalme Mtarajiwa … (Chanzo: France 24 / AFP 05/04/2018), na kutotia saini kandarasi hizo pia kulisababisha fedheha kwa kasri la Elysee: "Kwa upande mwengine, duru za kidiplomasia za Ufaransa ziliiambia shirika la habari la France 24 kuwa Ufaransa "haifuatilii kandarasi za kibiashara na Saudi Arabia kama ilivyokuwa nyuma, bali inatafuta kujenga ushirika wenye maono sawa yaliyo jengwa kwa msingi wa maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia ya muda mrefu". (Chanzo: AFP, 08/04/2018)

5) Kutokana na yote hayo juu, ili kuitendea haki ziara hiyo, kuna makubaliano ambayo tayari yashatiwa saini, makubaliano yaliyouteka moyo wa Bin Salman; makubaliano hayo yalitiwa saini kuasisi bendi ya kitaifa na jumba la burudani, wapi huko? Katika ardhi ya Misikiti miwili Mitukufu!! Waziri wa Utamaduni wa Ufaransa Françoise Nyssen alisema Paris itaisaidia Riyadh kuunda bendi na kujenga jumba la burudani," Nyssen alisema haya baada ya kutia saini makubaliano na Waziri wa Utamaduni na Habari Awad al-Awad jijini Paris. (Chanzo: tovuti ya Arab World mnamo 09/04/2018 (© REUTERS / POOL)

Bin Salman kabla ya makubaliano haya alifanya ziara mnamo Jumapili kabla ya ziara yake rasmi, alihudhuria tamasha la sherehe za Pasaka kusini mwa Ufaransa: Mwana wa Mfalme Salman aliwasili mnamo Jumapili 08/04/2018 akitokea Amerika. Anahudhuria tamasha la sherehe za Pasaka katika mji wa Aix-en-Provence karibu na mji wa Marseille kusini mwa nchi hiyo kufurahia mziki wa waandishi wa kale Debussy, Robert Schumann na Felix Mendelssohn. (Chanzo: AFP 08/04/2018)

6) Kwa hivyo ziara hiyo haikuwa na maana si kwa upande wa makubaliano wala kwa upande wa kandarasi, isipokuwa ikiwa jumba hilo la burudani litachukuliwa kuwa na maana, twajilinda na Allah kutokana na hili! Hili lilikuwa dhahiri katika mkutano wa mwisho wa waandishi habari uliofanywa mnamo Jumanne 10/4/2018, na kuchapishwa katika vyombo vya habari mnamo 11/4/2018. Ulieleza kuwa mikataba na makubaliano ya makusudi iliafikiwa, isipokuwa ya jumba la burudani, tayari ishatiwa saini! Mtandao wa Aljazeera net ulichapisha mnamo 11/4/2018: Mfalme mtarajiwa wa Saudia Mohammad Bin Salman alitamatisha mnamo Jumanne ziara ya siku mbili nchini Ufaransa kwa kutia saini kandarasi za makubaliano 19 baina ya Ufaransa na kampuni za Kisaudi zenye jumla ya thamani ya zaidi ya dolari bilioni 18. Makubaliano hayo yaliyo afikiwa yanahusu sekta za viwanda kama kemikali za petroli na matibabu ya maji, vile vile utalii, utamaduni, afya

Endelea Uk..16

na kilimo … miongoni mwa makubaliano makubwa ni tangazo la kampuni ya mafuta ya Kisaudi ya Aramco, la kutia saini makubaliano yenye thamani ya zaidi ya dolari bilioni 12 pamoja na kampuni za Kifaransa, zikiwemo, Total, Technip na Suez ya kuunda kwa pamoja kiwanda cha kemikali za petroli eneo la Jubail (Mkoa wa Kaskazini wa Saudi Arabia), ambao kampuni za Kifaransa zinamiliki kiwanda kikubwa zaidi cha kusafisha mafuta duniani. Hata makubaliano haya na Aramco hayakufungika tu na kuimarisha biashara ya Aramco, bali yanaangazia zaidi juu ya kuimarisha mapato ya kifedha ya kiwanda hicho cha usafishaji mafuta cha Kifaransa.

Hili pia liliripotiwa na shirika la habari la AFP mnamo 11 Aprili 2018, kutoka katika mkutano huo wa waandishi habari. Duru hiyo pia inasema: "Mwishoni mwa ziara ya Mfalme Mtarajiwa wa Saudi nchini Ufaransa mnamo Jumanne, nchi hizo zilitia saini kandarasi za makubaliano 19 baina ya kampuni za Kifaransa na za Kisaudi zenye jumla ya thamani ya zaidi ya dolari bilioni 18. Barua hizo za maafikiano zinahusu sekta za viwanda kama vile kemikali za petroli na matibabu ya maji, vile vile utalii, utamaduni, afya na kilimo, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na baraza la kibiashara kati ya Ufaransa na Saudia, linalo jumuisha waajiri na wawakilishi wa serikali zote mbili".

Katika mkutano huo wa waandishi habari, Macron na Bin Salman walitaja kadhia za kawaida kama vile Iran, makubaliano ya nuklia, Syria, Yemen, nk. pasi na kufafanua suluhisho halisi la kadhia hizi.

**Nne: Tamati:**

Tunarudia yale tuliyo yasema juu: Ziara kuu ni ile ya kwenda Amerika; ziara yake ya Uingereza ni ziara ya maliwazo kwa sababu ya kuchukua kwake hatua kali dhidi ya vibaraka wake (Uingereza) nchini Saudi Arabia. Ziara yake nchini Ufaransa ni ziara ya pembeni ya kujenga mazingira ya umaarufu kwa Bin Salman, ili isemekane kuwa alizuru nchi kuu barani Amerika na Ulaya.

**24 Rajab 1439 H**
**11/4/2018 M**